**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS-TAMISEMI**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MKURANGA**

**SHULE YA SEKONDARI MWINYI**

S.l.p 115, Mkuranga Baruapepe: mwinyisecondaryscool@gmail.com Simu: 0686975323

**Kumb Na. MSS/MDC/JIF/F V//VOL.1/2024/2025**

Mzazi / Mlezi wa……………………………………
S. L. P………………………
……………………………...

**YAH: TAARIFA YA MWANAO KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO MWAKA 2024/2025 SHULE YA SEKONDARI MWINYI**

**1.0 UTANGULIZI**

Nafurahi kukutaarifu kuwa, mwanao amechaguliwa kujiunga na **KIDATO CHA TANO MWAKA 2024/2025** na atasoma tahasusi (Combination) ya ...........................Hivyo, anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **01/07/2024**. Mwisho wa kuripoti ni tarehe **14/07/2024.** muda wa kuripoti ni kuanzia saa **7:30** asubuhi hadi saa 12:00. Aidha, mwanafunzi aripoti shule akiwa **amevaa sare ya shule.** Ni imani yetu mwanafunzi ataitumia nafasi hii adhimu kusoma na kujifunza kwa bidii na kwa uwezo wake wote pamoja na kushirikiana na wenzake, walimu na jumuiya nzima ya Mwinyi ili kulinda heshima na sifa ya shule kwa maendeleo yake na Taifa kwa ujumla.

**2.0 MAHALI SHULE ILIPO**

Shule ya Sekondari Mwinyi ipo kata ya **Mkuranga**, tarafa ya **Mkuranga**, Wilaya ya **Mkuranga** mkoa wa **Pwani**. Umbali wake ni km **45** kutoka kituo cha mabasi Mbagala mkoa wa Dar es Salaam. Shule ipo kando ya barabara kuu iendayo mikoa ya kusini ya Lindi na Mtwara. (Usafiri wa pikipiki Tsh 1000/= na bajaj Tsh 500/=) wa kukufikisha shuleni unapatikana katika kituo kikuu cha mabasi cha Mkuranga "**Mkuranga Bus Terminal**"

**3.0 KICHOKOO CHA SHULE "SCHOOL MOTTO"**

Kichokoo cha shule (school motto") ni tamko rasmi linaloelekeza au kutoa mwelekeo wa shule. Kichokoo cha Shule ya Sekondari **Mwinyi** ni **"NIDHAMU NA TAALUMA" (***DISCIPLINE AND ACADEMICS***)**. Ukiwa mwanafunzi wa shule hii tunatarajia utakuwa na nidhamu ya hali ya juu itakayokuwezesha kujijenga kitaaluma na ufanisi mkubwa na hivyo kuweza kujikomboa kimaisha na kuwa mtaalamu /raia mwema wa Taifa la kesho.

**4.0 MAHITAJI YA SHULE**

**A. SARE ZA SHULE**

i. Mwanafunzi aje na Suruali mbili za dark blue (zenye marinda mawili mbele kila upande na upana wa chini uwe inchi 14-16, zenye urefu unaofika kifundo cha miguu). Aidha, suruali za jinzi (Jeans) au zenye mitindo tofauti (modo) haziruhusiwi kuvaliwa kama sare za shule
ii. Shati mbili nyeupe zenye mikono mirefu (Aje nazo mwanafunzi mwenyewe)

iii. Mwanafunzi aje na suruali za kaki mbili zenye vipimo na vigezo vilivyoainishwa kwenye kipengele (i) pamoja na fulana (T-shirt) ya kijivu ambayo haina kola. Atakuwa anavaa suruali hizo siku ya Jumamosi, Jumapili na wakati wote usio wa masomo.

iv. Mwanafunzi awe na fulana ya kijivu (Tshirt yenye kola) yenye nembo ya shule atakayovaa kila siku ya Jumatano. (Zinapatikana mita 300 kutoka eneo la shule)

v. Mwanafunzi wa tahasusi ya **CBG** aje na koti la maabara

vi. Mkanda mweusi, viatu vyeusi vyenye visigino vifupi (gidamu) soksi nyeusi jozi mbili, sweta ya rangi dark blue yenye msuko wa V mbele na iwe na ufito mweupe shingoni, mikononi na chini, nguo za michezo (Track suit za dark blue na jezi za timu ya Taifa ya Tanzania kama inavyoonekana kwenye kielelezo cha picha katika ukurasa wa mwisho wa fomu hii)

vii. Lazima kuja na chandarua, shuka mbili za light blue, mto, foronya, ndoo mbili ndogo za lita 10, Sahani, Bakuli, kikombe, kijiko **(Sahani, bakuli na kikombe viwe vya udongo au mfupa)** na vifaa vingine vya usafi wa mwili. Unaweza kuvinunua Mbagala au Mkuranga ili kupunguza usumbufu.

viii. vii. Kila mwanafunzi aje na godoro lake lenye upana wa **futi 2.5**. (**Magodoro yaliyotumika yachukuliwe kwa tahadhari, ili kuepuka wadudu wasumbufu kama kunguni).**

## 5.0 MAHITAJI MENGINE MUHIMU SANA

| NA | MAELEZO | KIASI |
|---|---|---|
| **i.** | Mchango wa uendeshaji wa shule | 65,000/= |
| **ii.** | Tahadhari | 5,000/= |
| **iii.** | Kitambulisho cha shule | 5,000/= |
| **iv.** | Nembo | 5,000/= |
| | **JUMLA** | **80,000/=** |

**Tanbihi**

- Fedha yote katika kipengele nambari **(i – iv)** ilipwe **NMB A/C NO. 22801200027** jina la akaunti ni **THE HEADMASTER MWINYI SECONDARY SCHOOL.**
- Hatupokei fedha taslimu katika kipengele nambari (**i – iv**)
- Tumia hata mawakala wa NMB katika kupata huduma ya kuweka fedha.

## 6.0 VIFAA VYA DARASANI

a) Daftari kubwa 'counter books' 10 au zaidi
b) Mkebe wa hisabati na kikokotozi kwa tahasusi ya **CBG**
c) Advanced learners dictionary moja, rula yenye cm 30, kalamu za wino na penseli za kutosha.
d) Vitabu vya masomo vinavyo endana na Tahasusi yako (Orodha ya vitabu imeambatanishwa Pamoja na fomu hii)
e) Bunda la karatasi (ream A4) mbili kwa mwaka (utakabidhi).

## 7.0 VIFAA VYA KAZI NA USAFI

I. Kwa wanafunzi wa **CBG**, Aje na **Kwanja (1), Fagio la chelewa la wima (1) Jembe lenye mpini (1)**
II. Kwa mwanafunzi wa **HGK** Aje na **Kwanja (1), Softbroom (1)** na **Jembe lenye mpini (1)**
III. Kwa mwanafunzi wa **HGL, HGFa & HGLi**, aje na **Kwanja (1), Panga (1) Jembe lenye mpini(1)**

## 8.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. **25** ya mwaka **1978** na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. **10** ya mwaka **1995**. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

**8.1 Sheria na Kanuni za Shule**

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku ( **Preparation**)
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote ix. Kutunza mali za shule
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali.
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kukaa na dawa bila ya maelekezo na idhini ya daktari.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi. Mwanafunzi akitenda kosa hili anaweza kufukuzwa shule.**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**8.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa;
xi. Kusababisha mimba;
xii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;

xiv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xv. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**9.0 VIAMBATISHO NA FOMU MUHIMU**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**MWISHO**

a) Zingatia tarehe ya kufungua shule ili kuleta ufanisi kwenye kalenda ya masomo

**b) SIMU PAMOJA NA NGUO ZA NYUMBANI HAZIRUHUSIWI. KABLA YA KURUHUSIWA KUINGIA BWENINI UTAPEKULIWA**

c) Unatakiwa kuja na "**Result slip**" yako ya kidato cha nne na nakala ya cheti cha kuzaliwa.

d) **Zingatia:** Mwanafunzi aje shule akiwa amevaa suruali ya kaki na Tshirt ya kijivu isio na kola na maandishi yoyote (mikono mifupi)

e) Hakikisha unapima afya yako kwenye hospitali inayotambulika na serikali.

f) Kwa mawasiliano piga simu

**ZINGATIA**

**Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO:**

- ✓ **0686975323 Mkuu wa Shule** ✓ **0657476743/0754800345 Makamu wa Mkuu wa Shule**

**NB: MZAZI/MLEZI UNATAKIWA KULIPA MICHANGO YOTE KWA WAKATI**

**KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI MWINYI KWA ELIMU NA MALEZI BORA**

**.................................**

MAKUMBURA, H.S

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

## OFISI YA RAIS-TAMISEMI
## HALMASHAURI YA WILAYA YA MKURANGA
## SHULE YA SEKONDARI MWINYI

S.l.p 115, Mkuranga   Baruapepe: mwinyisecondaryschools0643@gmail.com   Simu: 0686975323

**Kumb Na. MSS/MDC/JIF/F V//VOL.1/2024/2025**   **Tarehe** ……………………………

**YAH: FOMU YA MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI (IJAZWE NA KURUDISHWA SHULENI)**

**SEHEMU A: (** *IJAZWE NA MWANAFUNZI MWENYEWE*)

1. Jina kamili la mwanafunzi (***majina matatu***)
2. Tarehe ya kuzaliwa (***Siku/Mwezi/ Mwaka***)
3. Mahali alipozaliwa (***kijiji/wilaya/mkoa***)
4. Uraia ____ Dini Dhehebu
5. Shule ya sekondari aliosoma ____ Namba ya Mtihani 6. Mahali unakotoka (kijiji/ wilaya/ mkoa)

**AHADI YA MWANAFUNZI**

Mimi _____________________________________________ Nikiwa na akili zangu timamu bila kushurutishwa ama kulazimishwa na mtu yeyote ninakubali nafasi niliyopewa ya kujiunga na kidato cha Tano.

"***Ninaahidi kutii kikamilifu sheria, taratibu na kanuni zote za shule wakati wote niwapo mwanafunzi wa SHULE YA SEKONDARI MWINYI***

**Sahihi ya mwanafunzi**…………………**Sahihi ya mzazi**................................   **TAREHE** ……………

**SEHEMU " B" – (** *IJAZWE NA MZAZI/MLEZI***)**

1. Jina la Mzazi/ mlezi
2. Kazi yako
3. Anuani/Simu
4. Mahali unapoishi
5. Namba ya NIDA

***PICHA YA MZAZI/MLEZI***

## 10.0 KIAPO CHA MZAZI/ MLEZI NA MWANAFUNZI CHA UTII WA SHERIA, KANUNI NA MIONGOZO YA SHULE

**Muhimu: Fomu hii ijazwe na Mzazi/mlezi wa mwanafunzi katika sehemu yake na Mwanafunzi ajaze sehemu yake na kasha irudishwe hapa shuleni siku ya kuripoti.**

### 10.1 SEHEMU : A (IJAZWE NA MZAZI AU MLEZI WA MWANAFUNZI)

---

(i) Mimi…………………………………………Mzazi/mlezi wa ………………………………. nakiri kwamba nimesoma, nimeelewa na ninakubali masharti yote yanayohusu mtoto wangu kujiunga na shule ya sekondari **MWINYI**. Nina ahidi **kwamba**

(ii) **Kwamba**, nitampatia mahitaji yote muhimu yaliyoainishwa katika fomu hii kama inavyotakiwa

(iii) **Kwamba**, nitalipa kwa wakati michango yote ya shule iliyoainishwa katika fomu hii

(iv) **Kwamba** nitashirikiana na uongozi wa shule na walimu wote wa shule hii katika malezi ya mwanangu ili aendelee vyema kinidhamu na kitaaluma

(v) **Kwamba** nitakuwa wa kwanza kumkanya, kumnasihi, kumuadhibu mwanangu au kumtia moyo na kumpongeza pale itakapobidi kufanya hivyo.

Sahihi ya Mzazi/Mlezi…………………………………………………………….

Tarehe………………………………

### 10.2 SEHEMU : B (IJAZWE NA MWANAFUNZI MWENYEWE)

Mimi ……………………………………………ambaye ni mwanafunzi, naelewa kwamba ni dhamana kubwa kwangu kupatiwa nafasi hii katika shule ya sekondari **MWINYI**. Baada ya kusoma masharti ya kujiunga katika shule hii nina ahidi kwamba

i) Nitafuata sheria, kanuni, taratibu na miongozo yote kama ilivyooelekezwa katika shule hii

ii) **Kwamba** nitakuwa mwenye bidii katika taaluma ili kufikia malengo ya uwepo wangu hapa shule

iii) **Kwamba** nitakuwa mstari wa mbele katika kuonesha nidhamu ya hali ya juu hata kuwa kiigizo chema kwa wanafunzi wenzangu

iv) **Kwamba** nitahudhuria shule mapema kila siku na kufanya shughuli zote za kitaaluma darasani na nje ya darasa

v) **Kwamba** sitashiriki katika maasi ya aina yoyote, sitajiunga na aina yoyote ya vikundi viovu

vi) vi) **Kwamba** nitakuwa mstari wa mbele katika kukemea na hata kuripoti matukio au vitendo vyote vyenye viashiria vya utovu wa nidhamu, uvunjifu wa amani na mfano wa haya ambavyo vinaweza kuleta taharuki na madhara makubwa kwa shule, jamii na taifa kwa ujumla

**Sahihi ya mwanafunzi**……………… **Tarehe**………………………

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
PO RALG
**MKURANGA DISTRICT COUNCIL**
**MWINYI SECONDARY SCHOOL**

P.o.box 115, Mkuranga Email: Mwinyisecondaryschool0643@gmail.com Hotline:+255686975323

Ref………………………………………………………………………………… (NAME OF STUDENT)

Please examine the named student as per medical examination form below,

**MAKUMBURA, H.S**
**THE HEADMASTER**

---

## MEDICAL EXAMINATION FORM

(To be completed by Government Medical Officer)

Full Name…………………………………………………………………………………….. ……........ ……

Age [ ] (Years) Height [ ] (cm) Weight [ ] (kg)

i Blood count (Red and White)……………………………………………………………………………………

ii Stool Examination……………………………………………………………………………………

iii Urinary analysis…………………………………………………… ……………………………………

iv STDS and other V.D ………………………………… ……………………………………………………

v T.B and Leprosy test……………………………………………………………………………………

vi Eye test……………………………………………………………………………………

vii Ear test……………………………………………………………………………………

viii Chest ……………………………………………………………………………………

ix Abdominal test……………………………………………………………………………………

x Blood Group……………………………………………………………………………………

xi Spleen……………………………………………………………………………………

Any additional defects or impairments, infections, chronic or family diseases ( e.g Sickle cell),

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

I have examined the above-named student and I certify that he/she is FIT/NOT FIT to pursue Secondary Education.

Signature…………………………….Date…………………. ……………………………

Station……………………………………………………………………………………………………

**Designation and Official Stamp……………………………………………………………………………**

ORODHA YA VITABU

TANBIHI:

- ✓ KILA MWANAFUNZI ANUNUE KULINGANA NA TAHASUSI (COMBINATION) ALIYOCHAGULIWA
- ✓ WANAFUNZI WOTE KWA KILA TAHASUSI NI LAZIMA WASOME SOMO LA GS
- ✓ VITABU VYA BASIC APPLIED MATHEMATICS NI KWA WALE WANAOSOMA TAHASUSI (COMBINATION) YA CBG TU.
- ✓ NUNUA VITABU KULINGANA NA UWEZO WAKO KATIKA KILA SOMO (SIO LAZIMA KUNUNUA VITABU VYOTE VILIVYOORODHESHWA KAMA UWEZO NI MDOGO)

GENERAL STUDIES

i JOANNNES BIGIRWAMUNGU (etalal)5thEdition 2019 UNDERSTANDING GERERAL STUDIES FOR ADVANCED LEVEL APE DSM.
ii NYAMBARI NYANGWINE UNDERSTANDING GENERAL STUDIES NOTED BOOK.
iii MBALASE BOOK 1 & 2
iv GENERAL STUDIES FOR V & VI BY MWAIPAJA M (2018)

CHEMISTRY

i CONCEPTUAL CHEMISTRY, DR.S.K.JAIN (S.CHAND) I & II
ii PHYSICAL CHEMISTRY FOR ADVANCED LEVEL SECONDARY SCHOOL-TIE (2019)
iii ORGANIC CHEMISTRY FOR ADVANCED LEVEL SEC. SCHOOL –TIE (2019)
iv INORGANIC CHEMISTRY FOR ADVANCED LEVEL SE.SCHOOL-TIE (2019)
v GENERAL CHEMISTRY FOR ADVANCED LEVEL SEC.SCHOOL –TIE (2019)
vi RAYMOND CHANG GENERAL CHEMISTRY.

BIOLOGY

i BIOLOGY SCIENCE BY SOPER
ii TIE FORM 5 & 6 BIOLOGY FOR ADVANCED LEVEL SEC.SCHOOL.
iii UNDERSTANDING BIOLOGY GLENN & SUZAN TOOTE.

GEOGRAPHY

i HUMAN AND ECONOMIC GEOGRAPHY BY GOH CHONG LEONG, GILLIAN C.MORGAN
ii GEOGRAPHY ,AN INTERGRATED APROACH BY DAVID WAUGH.
iii PRACTICAL GEOGRAPHY BY PITCHERD.
iv ELEMENTARY PHYSICAL GEOGRAPHY BY AHMED LUBWAMA.
v MAPSHEET KUBWA.

BASIC APPLIED MATHEMATICS

i TIE-BASIC APPLIED MATHEMATICS.

ENGLISH LANGUAGE

i A BEAUTIFUL ONES ARE NOT YET BORN BY AYI KWEYAMA
ii A MAN OF THE PEOPLE BY CHINUA ACHEBE
iii HIS EXALLENCE THE HEAD OF STATE BY DANSAFO
iv THE WONDERFUL SUGEON BY CHARLES MLOKA
v BETRAYAL IN THE CITY BY FRANCIS IMBUGA
vi AN ENERMY OF THE PEOPLE BY ERICK IBSEN
vii A COMPLETE COURSE IN COMMUNICATION SKILLS BY KADEGHE
viii I WIL MARRY WHEN I WANT BY NGUGI WA THION'G & NGUGI WAMII
ix THE REAL ENGLISH TEXT BOOKS FOUR ADVANCED BY KADEGHE 2010.
x SELLECTED POEMS BY TIE
xi THE OXFORD ADVANCED LEARNERS DICTIONARY
xii ADVANCED LEVEL ENGLISH A PRACTICAL APPROCH BY NICHOLOUS ACHERY.

HISTORY

i ESSENTIAL ISSUE HISTORY PAPER 1 & II BY YASIN
ii MAJOR ISSUES IN HISTORY I & II BY YASIN.

KISWAHILI

i KISWAHILI -1 (KIDATO CHA 5 & 6 ) BY KILANGI ENOCK LUCAS
ii KISWAHILI -2 (NADHARIA YA FASIHI) KIDATO CHA 5 & 6.BY KILANGI EN
iii KISWAHILI -2 (TAHAKIKI YA KISWHILI) KIDATO CHA 5 & 6 .BY KILANGI E LUCAS.
iv THAKIKI YA KISWAHILI - BY NYAMBARI NYANGWINE.
v CHUNGUTAMU MWANDISHI - T.A.MVUNGI
vi FUNGATE YA UHURU- MOHAMED SEIF KHATIB
vii KIMBUNGA- HAJI G.HAJI
viii MAPENZI BORA - SHAABAN ROBART
ix VUTA N'KUVUTE -SHAFI ADAM SHAFI
x MFADHILI - HUSEIN TUWA
xi USIKU UTAKAPOKWISHA - MBUNDA MSOKILE
xii KUFIKIRIKA - SHAABAN ROBART
xiii KIVULI KINAISHI - SAID MOHAMED
xiv NGUZO MAMA- PENINA MUHANDO
xv MORANI - EMMANUEL MBOGO
xvi KWENYE UKINGO WA THIM -EBRAHIM HUSSEIN.

mfgvjh



Sare ya darasani (Suruali na Shati la mikono mirefu)



Vazi la kushindia



Koti la maabara kwa mwanafunzi wa tahasusi (Combination) ya CBG



Sweta la bluu lenye ufito mweupe shingoni, mikononi na chini
(Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa nalo)